Dhambi Ya Nadab Na Abihu
(The Sin Of Nadab And Abihu)

Na

Ellis P. Forsman

Dhambi Ya Nadab Na Abihu

(The Sin Of Nadab And Abihu)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Dhambi Ya Nadab Na Abihu

Walawi 9:22-10:7

Agano la Kale linathamaani kubwa kwa Wakristo…

Imeandikwa kwa ajili ya kujifunza kwetu, chanzo kikuu cha taraja.

Rum. 15:4, "*Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini.*"

Iliandikwa ili kutufariji, ili kwamba tusifanye makosa kama hayo.

1 Kor. 10:11, "*Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mfano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani.*"

Hii inajumuisha hata kitaabu cha Mambo ya WALAWI. Kitabu kikavu kwa wengi, lakini lenye thamani kwa wote.

Jina la kitabu hiki kinatokana na LAWI, kabila lililotokana na makuhani.

Kimsingi ni kitabu kidogo cha makuhani chini ya Sheria ya Musa.

Kukisoma kunamsaidia Mkristo kuelewa vyema kitabu chaa Waebrania.

Hata kama kitabu kinaorodhesha kanuni za kikuhani, inaandika tukio linalowahusisha wana wa Aruni: Nadab na Abihu.

Kilichowatokea kinaweza kutupatia somo lenye thamani. Kilichotokea na tunachoweza kujifunza kitatumika kama msingi wa somo hili.

Tuanze na kusoma kuhusu…

Tukio linalowahusisha Nadab na Abihu

Mazingira yanayopelekea matendo yao…

Kuwekwa wakfu kwa Haruni na wanawe kama makuhani imemalizika kwa muda mfupi (Walawi, sura za 8 & 9).

Katika Walawi 9:22-24, utukufu wa Bwana ulionekana wakati Haruni alipowabariki watu.

Law. 9:22-24, "*Kisha Haruni akainua mikono yake na kuielekeza kwa hao watu, akawabariki kasha akashuka akisha isongeza sadaka ya dhambi, na sadaka ya kuteketezwa, na sadaka ya*

amani. Kasha Musa na Haruni wakaingia ndani ya hema ya kukutania, kasha wakatoka nje, na kuwabariki watu; na huo utukufu wa BWANA ukawatokea watu wote. Kisha moto ukatoka hapo mbele za BWANA, na kuiteketeza sadaka ya kuteketezwa, na yale mafuta juu ya madhabahu; watu wote walipouona huo moto wakapiga kelele wakainama kifudifudi."

Moto ukatoka hapo mbele za Bwana.

Moto ukaiteketeza maafuta na mafuta.

Watu wakapiga kelele na kuinama.

Moto wa kigeni uliotolewa na Nadab na Abihu – Walitwaa moto ambao Bwana hakuwaagiza.

Law. 10:1, "*Na Nadab na Abihu wana wa Haruni wakatwaa kila mtu chetezo chake, wakatia moto ndani yake wakatia na uvumba, nao wakatoa moto wa kigeni mbele ya BWANA, ambao yeye hakuwaagiza.*"

Unaitwa moto wa "*kigeni*".

Tafsiri ya NIV inaitafsiri moto "*moto ambao hawakuagizwa.*"

Ni mhimu kukumbuka kwamba ilikuwa ni kitu ambacho Bwana hakuagiza!

Moto ukatoka mbele za Bwana na kuwala.

Law. 10:2, "*Kisha moto ukatoka hapo mbele za BWANA, nao ukawala, nao wakafa mbele za BWANA.*"

Mungu aliukubali moto katika Law. 9:24, lakini akaukataa moto katika Law. 10:2

Huo moto mwingine uliashiria baraka za Mungu; lakini moto mwingine uliashiria, laana ya Mungu.

Kwa nini Mungu hakupendezwa? Maelezo kadhaa imetolewa:

Waliweka makaa yaanayowaka katika chetezo ambayo haikuwa katika madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa.

- Law. 16:12, "*Kisha atatwaa chetezo kilichojaa makaa ya moto yatokayo katika madhabahu iliyo mbele za BWANA, na konzi mbili za uvumba mzuri uliopondwa sana mikononi mwake, naye atauleta ndani ya pazia.*"
- Kut. 30:9, "*Hamtafukiza juu yake uvumba mgeni, wala sadaka ya kuteketezwa, wala sadaka ya unga, wala hamtamimina juu yake sadaka ya kinywaji.*"

Katazo dhidi ya vinywaji vilivyo changanywa iliyofuata inawafanya watu kuamini kwamba yawezekana walilewa.

Law. 10:8-10, "*Kisha BWANA akanena na Haruni na kumwambia, usinywe divai wala kileo cho chote, wewe, wala wanao pamoja nawe, hapo mwingiapo ndani ya hema ya kukutania, ili kwamba msife; amri hii itakuwa ni amri ya milele katika vizazi vyenu; kasha mpate kupambanua kati ya yaliyo matakatifu, na hayo yaliyo ya siku zote, na kati ya yaliyo najisi na hayo yaliyo safi.*"

Jaribio lao la kutaka kuingia mahali Patakatifu kwa wakati usiyofaa.

Law. 16:1-2, "*BWANA akasema na Musa baada ya kufa kwa hao wana wawili wa Haruni, walipokaribia mbele za BWANA, wakafa; BWANA akamwambia Musa, sema na Haruni ndugu yako, kwamba asiingie wakati wowote katika mahali patakatifu ndani ya pazia, mbele ya kiti cha rehema, kilicho juu ya sanduku, asije akafa; maana mimi nitaonekana katika lile wingi juu ya kiti cha rehema.*"

Dhambi yao inaweza kuwa ni muunganiko wa mambo haya, lakini msitari wa kwanza inasema kwamba ilikuwa ni kufanya kile ambacho Mungu hajakiagiza.

Maelezo ya Musa kwa kilichotokea...

Wale wamkaribiao Mungu lazima wamchukulie kama "*takaswa*", au "*mtakatifu*".

Law. 10:3, "*Ndipo Musa akamwambia Haruni, jambo hili ni hilo BWANA alilolinena, akisema, nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, name nitatukuzwa mbele ya hao watu wote. Haruni akanyamaza kimya.*"

"*kutakaswa*" inamanisha "kutengwa, wekwa wakfu"; n.k., kuhudumiwa kama maalum.

Kiualisia, tukio la Nadab na Abihu haikumheshimu Mungu.

Ni lazima Mungu "*atukuzwe*" kabla ya yote.

Law. 10:3, "*Ndipo Musa akamwambia Haruni, jambo hili ni hilo BWANA alilolinena, akisema, nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, name nitatukuzwa mbele ya hao watu wote. Haruni akanyamaza kimya.*"

Neno hili linamaanisha "*kutii*".

Tendo la Nadab na Abihu hivyo bassi halikumtii Mungu.

Maelekezo zaidi ya Musa.

Miili ya Nadab na Abihu kutolewa nje ya madhabahu.

Law. 10:4-5, "*Musa akawaita Mishaeli na Elisafani, wana wa Uzieli mjombaye Haruni na kuwaambia, njooni karibu mwachukue hawa ndugu zenu, mkawaondoe hapa mbele ya maskani, mwende nao nje ya marango. Basi wakaja karibu na kuwachukua, haali wamevaa nguo zao, wakawachukua nje ya marango; kama Musa alivyosema.*"

Haruni naa wanawe waliopona hawakupaswa kuhuzunika wakati walipokuwa wangali wamewekwa wakfu kwa ajili ya huduma.

Law. 10:6-7, "*Kisha Musa akamwambia Haruni na wanawe Eleazari na Ithamari, msiache wazi nywele za vichwani mwengu, wala msiyararue mavao yenu; ili kwamba msife, tena asiukasirikie mkutano wote; lakinin ndugu zenu nyumba yote ya Israeli, na waomboleze kwa ajili ya hicho kichomo alichowasha BWANA. Wala hamtatoka mlangoni mwa hema ya kukutania, msije mkafa; kwa sababu mafuta ya kutiwa ya BWANA ya juu yenu. Nao wakafanya kama hilo neno la Musa.*"

Ingeweza kuwa vigumu kwa Haruni kuwapoteza vijana wake wawili kwa njia hii, kwa tukio ambalo lingeweza kuwa ni wakati wa furaha kuu kwake.

Kwa vile mambo haya yaliandikwa kwa ajili ya kutuonya (1 Kor. 10:11), ni somo gani linaweza kuwepo kwa ajili yetu?

Somo ambalo linapaswa kuegemewa katika tukio hili

Kuzingatia ibada ya Mungu.

Tunapomkaribia Mungu kwa ibada, tunapaswa kufanya tu alichoagiza.

Hili lilikuwa ni kosa lililofanywa na Nadab na Abihu.

Law. 10:1, "*Na Nadab na Abihu wana wa Haruni, wakatwaa kila mtu chetezo chake, wakatia moto ndani yake, wakatia na uvumba, nao wakatwaa moto wa kigeni mbele za BWANA, ambao yeye hakuwaagiza.*"

Tunapotoa kile ambacho Mungu hajaagiza...

Hatumchukulii kama "ametakaswa" au "mtakatifu".

Law. 10:3, "*Ndipo Musa akamwambia Haruni, jambo hili ni hilo BWANA alilolinena, akisema, nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, nami nitatukuzwa mbele ya hao watu wote. Haruni akanyamaza kimya.*"

Hakika hatumtukuzi.

Law. 10:3, "*Ndipo Musa akamwambia Haruni, jambo hili ni hilo BWANA alilolinena, akisema, nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, nami nitatukuzwa mbele ya hao watu wote. Haruni akanyamaza kimya.*"

Kama Mungu ni mtakatifu na hakika anafaa utukufu...

Mwenye dhambi atajuaje anachokipenda Mungu kama ibada inayokubalika?

Je mwenye dhambi anaweza kusoma mawazo ya Mungu?

Kama ndivyo, basi Mungu siyo mtakatifu (tengwa)!

Kama ndivyo, basi Mungu hatofautiani na mwanadamu na hivyo hapaswi kutukuzwa?

Hakika, mwanadamu hawezi kuelewa pasipo ufunuo wa kipekee ambavyo Mungu anataka aabudiwe na kutukuzwa isipokuwa akituambia.

Isa. 55:8-9, "*Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA. Kwa maana kama vile mbingu zilivyojuu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.*"

Hii ndiyo sababu inayotufanya tusitumie vyombo vya muziki katika ibada.

Katika Agano Jipya, kuimba pekee imeahinishwa.

- Efe. 5:19, "*Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu;*"
- Kol. 3:16, "*Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani mwenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.*"

Kutoa sifa kwa vyombo vya Muziki...

- Kinaweza kuwa kitu ambacho Mungu hajaagiza.
- Inaweza kuwa maksudi kwa upande wetu.

Kufanya hivyo kunaweza kufanya kumbashiri Mungu wa pili.

- Kama Mungu alitaka hivyo, angetuambia.
- Kwa vile hakutuambia, tunamheshimu kwa kutoa kile alichotuamuru tu.

Hii ndio sababu tunatumia kikombe kimoja tu katika meza ya Bwana.

Katika Agano Jipya, kikombe kimoja pekee ndio kimesemwa.

- Mat. 26:27-28, "*Akakitwaa kikombe akashukuru, akawapa akisema, nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi.*"
- Marko 14:23-24, "*Akatwaa kikombe akashukuru, akawapa, wakakinywea wote. Akawaambia hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi.*"
- Luka 22:14-21, "*Hata saa ilipofika aliketi chakulani, yeye na wale mitume pamoja naye. Akawaambia nimetamani sana kula pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu; kwa maana nawaambia ya kwamba siili tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu. Akapokea kikombe akashukuru akasema, twaeni hiki mgawanye ninyi kwa ninyi; maana nawaambia tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja. Akatwaa mkate akashukuru, akaumega, akawapa akisema, huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kula; akisema, kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu inayomwagika kwa ajili yenu. Walakini tazama mkono wake yeye anayenisaliti upo hapa pamoja nami mezani.*"
- 1 Kor. 10:16-17, "*Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja.*"

Kwa vile Bwana tayari ameshaeleza kwamba tunatumia kikombe kimoja, angeweza tu akaongeza msitari mwingine katika kifungu hicho hapo juu:

"*Sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja.*"

1 Kor. 11:25-28, "*Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu, na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate na kukinywea kikombe.*"

Kuzingatia nafasi ya Mungu…

Huduma kwa Bwana inakuja kabla ya huduma kwa familia zetu.

Hii tunajifunza wakati Haruni alipozuiwa kuomboleza kwa ajili ya wanawe.

Ilikuwa mhimu kwa wengine kutoa miili nje ya madhabahu.

Law. 10:4-5, "*Musa akawaita Mishaeli na Elisafani, wana wa Uzieli mjombaye Haruni na kuwaambia, njooni karibu mwachukue hawa ndugu zenu, mkawaondoe hapa mbele ya maskani, mwende nao nje ya marango. Basi wakaja karibu na kuwachukua, haali wamevaa nguo zao, wakawachukua nje ya marango; kama Musa alivyosema.*"

Haruni alitakaswa, na huduma kwa Bwana ilikuwa ya kwanza.

Law. 10:6-7, "*Kisha Musa akamwambia Haruni na wanawe Eleazari na Ithamari, msiache wazi nywele za vichwani mwengu, wala msiyararue mavao yenu; ili kwamba msife, tena asiukasirikie mkutano wote; lakinin ndugu zenu nyumba yote ya Israeli, na waomboleze kwa ajili ya hicho kichomo alichowasha BWANA. Wala hamtatoka mlangoni mwa hema ya kukutania, msije mkafa; kwa sababu mafuta ya kutiwa ya BWANA ya juu yenu. Nao wakafanya kama hilo neno la Musa.*"

Yesu alitoa kauli kama hiyo katika matukio kadhaa.

Alipokuwa akiwaita watu wamfuate.

Luka 9:59-62, "*Akamwambia mwingine, nifuate. Akasema Bwana nipe ruhusa kwanza niende nikamzike baba yangu. Akamwambia, waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu. Mtu mwingine pia akamwambia, Bwana nitakufuata; lakini nipe ruhusa kwanza nikawaage watu wa nyumbani mwangu. Yesu akamwambia, mtu aliyetia mkono wake kulima kasha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu.*"

Alipowahutubia watu wengi waliomfuata.

Luka 14:25-33, "*Makutano wengi walipokuwa wakifuatana naye, aligeuka akawaambia, kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam na hata nafsi yake mwenyewe; hawezi kuwa mwanafunzi wangu. Maana ni nani katika ninyi kama akitaka kujenga mnara, asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anavyo vya kuumaliza. Asije akashindwa kuumaliza baada ya kuupiga msingi, watu wote waonao wakaanza kumdhihaki, wakisema mtu huyu alianza kujenga, akawa hana nguvu za kumaliza. Au kuna mfalme gani akitaka kwenda kupigana na mfalme mwingine, asiyeketi kwanza na kufanya shauri, kwamba yeye pamoja na watu elfu kumi ataweza kukutana na yule anayekuja juu yake na watu elfu ishirini.? Na kama akiona hawezi, hutuma ujumbe kutaka sharti za amani, mtu yule akali mbali. Kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.*"

Alipowaandaa mitume wake kwa ajili ya kazi yao.

Mat. 10:34-37, "*Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! Sikuja kuleta amani, bali upanga. Kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu; na adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake. Apendae baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili.*"

Mfutano unapotekea kati ya huduma kwa Bwana na majukumu ya familia, Kristo lazima awe wa kwanza!

Mfano: kutii injili bila kujali kukataliwa na wanafaamilia.

Au: Kuweka kusanyiko la kanisa la Bwana kuwa la kwanza wakati kampuni inapokuja.

Hii aihitaji kwamba tuwe wakaidi kwa wageni wetu.

Wakaribishe waende na wewe, au waruhusu wajiandae nyumbani hadi utakaporudi.

Hiki ndicho inachomanisha "kutafuta kwanza ufalme wa Mungu na *haki yake*" (Mat. 6:33)

Hitimisho

Ni rahisi sisi kupotea katika huduma zetu kwa Mungu.

Hili linapotokea, inajitokeza katika ibada zetu na huduma kwa Bwana.

Tunapaswa kumchukulia kama Mtakatifu na tumtukuze kama anavyostahili kwa kufanya sawasawa na anavyoagiza.

Tunapoanza kutoa katika ibada JINSI tunavyotaka LINI tunataka, basi ibada yetu inakuwa ni ya kutaka mtu kuliko ya hatia!

Tunahitaji kukumbushwa matukio kama haya yaliyowatokea Nadab na Abihu...

- Kutunyenyekeza katika uwepo wa Mungu.
- Kutukumbusha umaana ya kumhudumia Mungu kwa njia aliyotuonyesha.

Je tunamchukulia Mungu kama mtakatifu, na kumtukuza vizuri katika huduma zetu kwake? Je tunamtumikia kwanza? Hata zaidi ya wale walioko karibu nasi?

Mfano wa Nadab na Abihu na itutie moyo kufanya kile kinacho mheshimu Mungu!